

Mafanikio ya ICANN

Kati ya mafanikio ya bivi karibuni ya ICANN ni: ICANN ilianzisha mashindano ya soko ya urajisi wa majina rejareja ya domeini (gTLD) yenye kusababisha kushushwa kwa gharama za jina la domeini kwa asilimia 80 na kuwezesha wateja na biashara kuokoa zaidi ya dola bilioni 1 za kimarekani kwa mwaka katika ada za urajisi.

ICANN iliandaa Sera Imara ya Utatuzi wa Mizozo ya Majina ya Domeini [Uniform Domain Name Dispute Resolution Policy (UDRP)], ambayo imetumika katika utatuzi wa zaidi ya mizozo 5000 inayohusu haki za umiliki wa majina ya domeini. UDRP imeundwa ili iwe ya ufanisi na yenye gharama ya chini.

ICANN, ikifanya kazi kwa ushirikiano na jamii hasusa za kiteknolojia na washikadau, ili waige kanuni za uandalizi wa Majina ya Kimataifa ya Domeini [Internationalized Domain Names (IDN)], na kuandaa mwanzo wa urajisi wa domeini kwa mamia ya lugha za ulimwengu.

Kazi ya ICANN Inayoendelea

Katika mwaka 2000, ICANN ili anzisha Domeini ya Kiwango cha Juu ya Madhumuni Rejareja [Generic Top Level Domain (gTLD)] saba mpya: .aero, .biz, .coop, .info, .museum, .name, na .pro.

Kwa wakati huu jumuiya ya ICANN inakagua uwezekano wa kuongeza gTLD za ziada. Katika juhudi za kutuliza wasiwasi wa jumuiya kuhusu ubepari na upatikanaji, ICANN inaandaa warsha kadhaa kuhusu 'Ni Nani?' [Whois], takwimu ya umma ya urajisi wa majina ya domeini.

Kukiwa na utumiaji wa IPv6, mfumo mpya wa kuweka namba za anwani za Itifaki ya Intaneti (IP), uendelezi bora wa mtandao wa ulimwengu utaendelea kuwa jitihada ya msingi ya ICANN.

ICANN Inakaribisha Ushirika

Kushiriki katika ICANN hakuna masharti kwa wote wenye nia ya kuhusika katika sera ya ulimwengu ya Intaneti kama inavyohusiana na jitihada ya ICANN ya usawazishaji wa kiufundi. ICANN inafanikisha kumbi nyingi katika mtandao ambazo zinapatikana kupitia mtandao wa ICANN, na Mashirika Wasaidizi na Kamati za Ushauri (Supporting Organizations and Advisory Committees) zina orodha barabara za mawasiliano ya washiriki. Zaidi ya hayo, ICANN huwa na mikutano ya umma wakati wote mwakani. Mikutano ya hivi karibuni imefanyika Bucharest, Montreal, Shanghai, Rio de Janeiro, na Accra.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mashirika Wasaidizi na Kamati za Ushauri, tafadhali tazama wavuti zao:

Address Supporting Organization (ASO)
www.aso.icann.org

Country Code Domain Name Supporting Organization (CCNSO)
www.ccnso.icann.org

Generic Names Supporting Organization (GNSO)
www.gnsso.icann.org

At-Large Advisory Committee (ALAC)
www.alac.icann.org

Governmental Advisory Committee (GAC)
www.gac.icann.org

Maelezo zaidi kuhusu ICANN yanapatikana katika mtandao wa ICANN:

<http://www.icann.org>

Internet Corporation for Assigned Names and Numbers
4676 Admiralty Way
Suite 330
Marina Del Rey CA 90292
USA
Simu: +1.310.823.9358
icann@icann.org



**Internet Corporation for
Assigned Names and Numbers
(Ushirika wa Intaneti wa Majina
na Namba Zilizo Awazishwa)**

*Jumuiya ya Ulimwengu ya Intaneti
inashirikiana kuimarisha uthabiti na
uadilifu wa Intaneti.*